# BWANA ALIPOTEMBEA KOTE KOTE ANGANI

MAONO YA AJABU YA MEI 17,2004




## UNYAKUZI WA KANISA

SIKU YA UNYAKUZI ndio ile siku *maalum* iliyotengwa na MUNGU MKUU MWENYEZI kama wakati tisha wakutoa hesabu wakati ambapo BWANA Yesu Atarudi kutoka mbinguni ili kihalisia Akaweze kulinyakuwa kanisa LAKE takatifu kutoka hapa duniani hadi kwa Ufalme wa mbinguni wa utukufu. Ni tukio la kisiri litakalo tendeka g*hafla, kwa kufumba na kufumbua jicho*, katika njia ipitayo ufahamu wa binadamu. Ni siku itakayokuja kama mwivi katikati ya usiku,bila ilani yoyote au tangazo la namna yoyote ile. Siku hiyo itakapofika,malango ya mbinguni yatafunguka ghafla, kisha kufuatwa na amri kuu, na Sauti ya malaika mkuu, na kisha mwito mkuu wa tarumbeta ya MUNGU. Hapo ndipo hatimaye BWANA Yesu atajiwasilisha mawinguni,na wafu ndani ya Kristo ambao kwa sasa wamelala katika mavumbi ya dunia wataamka.Hawa Wakristo wafu watakatifu watafufuka na kuwa wa kwanza kupaa angani, ili kukutana na BWANA mawinguni. Ni baada tu ya hapo ndipo, wale Wakristo watakao kuwa hai bado wakati wa unyakuzi, wakiwa waliishi maisha ya kiungu katika *utakatifu* kamilifu wakati huo, watainuliwa ili kuungana na wengine hewani, ili wakutane na BWANA angani.

### MAONO YA UNYAKUZI

Ni ya kustajaabisha sana kuwa pale awali katika mwaka wa 2004, BWANA MUNGU MKUU MWENYEZI wa mbinguni Alikuwa tayari Ameanza kushiriki pamoja nami juu ya swala hili la uzito la kuja kwa utukufu kwa Masihi, na maandalizi yanayohitajika. Ilikuwa katika hiyo siku isiyoweza husahaulika ya Mei,tarehe 17 mwaka wa 2004, ndipo BWANA Alipoamua kunena pamoja nami juu ya kuja kwake Masihi. Katika Maono hayo , Alinionyesha jinsi siku hiyo *iliotarajiwa* na ya kuogofya sana ya unyakuzi wa utukufu, wa kanisa takatifu la Kristo, itakavyotendeka. Yote yalitendeka katika maono ya usiku wakati BWANA

Alinisisitizia hitaji la kanisa kwenye pembe nne zote duniani kutubu, kutembea katika *utakatifu* na kujiandaa kwa *unyakuzi* wa utukufu. MUUMBA wa Israeli Alinionyesha maono hayo katika sehemu mbili hiyo Mei tarehe17 mwaka wa 2004 usiku. Sehemu ya kwanza ya huu mtembeleo ilikuwa ya kina sana kiasi ya kwamba ilinitoa pumzi. Hii ni kwa sababu katika hayo maono ya MUNGU, Nilijipata nikiwa nimesimama hapa chini duniani nikiwa natazama moja kwa moja juu angani. Ilikuwa nilipokuwa bado ninatazama anga, ndipo matukio yalipoanza kutendeka upande wa mkono wa kulia wa anga, katika njia ambayo haijawahi kuonekana kamwe. Katika huo upande wa kulia wa anga, kwa ghafla, pete za dhahabu katika njia ya mlazo zikajitokeza angani.Hizo pete mbili kuu za mlazo zilizotokea katika upande wa kulia wa anga zilikuwa za kunyambulika sana kiasi ya kwamba zilibadilishabadilisha umbo lake mara kwa mara. Kisha utukufu wa BWANA ukazipiga zile pete mbili za arusi zilipokuwa zikibadilishabadilisha umbo lao. Kila mara zilipogeuza umbo lake kwa njia ya mlazo ziliwekwa moja kando ya nyingine na kutoa umbo lililoonekana kama tarakimu 8 iloyoandikwa kwa mlazo. Hizo pete zenyewe zilitengenezwa kwa muundo wa kirauni, wa kidoti, wenye kupambwa vilivyo, kotekote kwenye nyuso zake.



## MILIPUKO WA TARUMBETA

Wakati haya yote yalipoendelea na hizo pete za utukufu za arusi, ndipo kwa ghafla SAUTI KUBWA ILIYOPAZWA kutoka mbinguni ikatokea na kunishtua zaidi ya sana. Baada ya hiyo sauti kubwa kutoka mbinguni, hapo ndipo nilipoisikia sauti kuu kutoka mbinguni ikitangaza katika upande huo wa mbali wa anga ikisema,

> TAZAMA! BWANA YU KARIBU KUTOKEA ANGANI."

Kisha utukufu wa MUNGU ukang'aa kwa kumetameta sana na kwa uzito kabisa katika huo upande wa kulia wa anga. Wakati huo, ufunuo mpya ulikuwa karibu kufunuliwa. Hii ilifuatwa mara moja na sauti ya mwito mkuu wa tarumbeta ya MUNGU MKUU MWENYEZI mbinguni. MILIPUKO YA TARUMBETA niliyoisikia, ilisikika katika huo upande wa mkono wa kulia wa anga zilipokuwa zile pete.

## TAJI YA UTUKUFU

Mahali hapa, Utukufu wa BWANA ulitokea kwa ghafla mahali pale pale zilipokuwa zile pete. Mahali hapo, MUNGU MKUU MWENYEZI Alinisababisha nijue ya kwamba matukio ya mwisho ya kilele yalikuwa karibu kutendeka angani. Hapo ndipo hatimaye BWANA Alitembea kutoka mbinguni hadi angani , na akasimama hapo moja kwa moja mbele yangu, Akinitazama. Ningeweza kuona kwa wazi kabisa TAJI YAKE YA KUPENDEZA Aliyovaa, na VAZI LAKE lililokuwa zaidi ya NYEUPE PE PE PE, ikiwemo ile nguo nyekundu iliyotoka begani mwake kutoka kulia hadi kushoto. Taji ambayo BWANA Alikuwa Amevaa, ilikuwa *ikimetameta* na utukufu mkuu sana wa dhahabu ya kitajiri na *mapambo* fulani mazuri ya kisamawati ipitayo ufahamu wa kibinadamu. Ile dhahabu ya kupendeza ya samawati, ya kitajiri iliyowekwa kwenye ile taji kwa hakika ilijitokeza na kudhihirisha sana mapambo yake. Hapo ndipo BWANA Alipouvuta umakinifu wangu kimakusudi karibu zaidi na TAJI YAKE KUU ya kwamba niweze kuitazama kwa wazi zaidi hata na kila kipengee kwa kina. Wakati huo, ndipo BWANA Alipouchukuwa mkono WAKE wa kushoto *uliyodungwa msumari* na kuunyosha kwangu ili kunionyesha zile *alama za msumari* kwenye huo mkono. Ile *alama ya msumari* niliyoiona kwa Mkono wa BWANA ilikuwa ya utukufu sana, sawa na Mkono WAKE. Punde tu BWANA MKOMBOZI wetu Alipokuwa na hakika kwamba nilikuwa nimemakinika kabisa kwa Mkono WAKE wa kushoto uliyodungwa msumari, hapo ndipo Alipoamua hatimaye kuuchukua huo Mkono na kuutumia kutengeneza TAJI YAKE YA UTUKUFU kichwani. Wakati huo, baada ya kuitengeneza TAJI YAKE ILIYOPAMBWA KWELI KWELI, ndipo BWANA Alipogeuka na kuangalia upande wa mkono wa kushoto wa anga, na kisha katika tukio la kustajaabisha sana, la kushangaza Akatembea kote kote angani kuelekea upande wa kushoto zaidi wa anga. Hili lilikuwa tukio la kushangaza zaidi ya yote, kuwahi kushuhudia katika maisha yangu yote. BWANA Yesu Masihi sasa kihalisia Akitembea kote kote angani kuelekea mwisho zaidi wa kushoto, huku nikitazama. Lakini, Alipokuwa Akitembea kwa ukuu kote kote angani, kilichonitetemesha zaidi na kunisababisha niogope, ilikuwa swala kwamba kila HATUA Aliyopiga angani , iliacha nyuma WAYO wa utukufu ambao ulimetameta sawa sawa kote kote angani. Zile NYAYO za utukufu ambazo BWANA Aliziwacha kotekote angani, zingeweza kufuatiliwa hadi kutoka upande wa kulia wa anga Alikoanzia safari YAKE. Jambo lingine la ajaabu ambalo nilitunikiwa kushuhudia, lilikuwa swala kwamba mara tu BWANA Alipotokea angani, inaonekana Alichukua hatamu kamilifu na ushukani kamili wa anga juu ya dunia,kiasi ya kwamba hakuna kitu kingine chochote kilikuwa cha umuhimu tena. Siku hiyo, nilipata kuonja kionjo kidogo tu cha kile ambacho utawala wa Masihi na mamlaka YAKE itahusisha. Hata hivyo, wakati BWANA hatimaye Alifika mwisho kabisa wa kushoto wa mwisho wa anga , Alisimama na Akageuka kuniangalia. Kisha mara moja akauchukua Mkono WAKE wa kulia *uliodungwa msumari* na Akatengeneza TAJI Aliyovaa. Akijua vyema kabisa kwamba sasa nilikuwa nimemlenga , ndipo BWANA Akauchukua Mkono wake wa kulia *uliyodungwa msumari* na kuunyosha kimakusudi kunielekea katika hatua iliyokusudiwa kunionyesha *alama za msumari* ambazo leo hii zinatia alama kwa Mkono WAKE wa kulia pia. Nikiwa bado katika mshangao na hofu ya ile *alama ya msumari* kwa Mkono WAKE wa kulia na utukufu iliyokuwa nao , hapo ndipo kwa ghafla ,BWANA Aligeuka, na mbingu ikafunguka na kihalisi Akatatembea moja kawa moja hadi mbinguni huku nikitazama. Ninakumbuka mahali hapa nikimulilia huku nikisema, 'BWANA, tafadhali nichukue niende na wewe.' Hisia na tajriba ya kuwa *karibu* sana NAYE na uwepo wake *kifizikia* ilikuwa kubwa zaidi sana kiasi kwamba hakuna mwanadamu yeyote awezae kuibadilisha na kitu kingine chochote hata kama ni kuu au ya bei ghali kiasi gani. Bado ninakumbuka bayana kabisa kwamba nilipomulilia Aende nami Mbinguni Alikokuwa Ametembea kuelekea, Machozi yangu yalidondoka Alipoingia, na Mawingu yakaanza kumfunika mle ndani.

Hapo ndipo MUNGU wa mbinguni Alininea kwa Sauti Akisema, 'TAZAMA, ANARUDI UPESI!' Ndipo nikaacha kufuatilia kwamba Anichukue NAYE. Lakini wakati huo, sasa nilibaki nimelenga anga na nilikuwa nimepigwa na butwaa na NYAYO za utukufu Alizoziwacha nyuma kotekote angani. Hapo ndipo nilipoamka na nilikuwa nimeshangaa sana na yale yaliyokuwa yamenitendekea tu, kiasi ya kwamba singejizuia. Nilizirai!

## UFUNUO

Wakati wa huduma YAKE yote ya hadharani hapa duniani, BWANA wetu Yesu Alikuwa mara kadha wa kadha Ameliahidi kanisa ya kwamba siku moja Angewaacha na kuenda kwa Nyumba ya BABA mbinguni, na kuwaandalia mahali. Katika ahadi hiyo inayosherehekewa sana ,BWANA Aligusia swala kwamba kuna vyumba vingi katika Nyumba ya BABA YAKE na ya kwamba Atachukua jukumu la kuandaa vyumba hivyo kwa ajili ya kanisa takatifu, la utukufu (Yohana 14:1). Ni ya ajaabu ya kwamba katika hatua ya kujitahidi kutimiza ahadi hii , siku moja Yesu Aliwapeleka wanafunzi WAKE kwa Mlima wa Mizeituni. Ni baada ya kuimaliza misheni yake ya kumukomboa mwanadamu, na kufufuka kwa utukufu kutoka kwa wafu, ndipo BWANA Yesu Aliwapeleka wanafunzi wake katika Mteremko wa Mashariki kwenye Mlima wa Mizeituni mahali paitwapo Bethania. Mahali hapo, Aliiniua juu Mikono YAKE *iliyodungwa msumari* kuwabariki, katika kile ambacho kingezingatiwa kuwa kauli YAKE ya kwaheri kwao. Lakini ilikuwa Akiwa bado katika hatua hiyo ya kuwabariki, ndipo Wingu la MUNGU likatokea na kumuinua juu katika Ufalme wa utukufu wa mbinguni. Hilo Wingu *lilimnyakua* BWANA Yesu waziwazi hadi mbinguni. KUNA maandiko dhahiri KADHA WA KADHA ambayo kando na kunakili ,pia yanasherehekea siku ya *unyakuzi* kwa hali ya juu sana kama siku ya muhimu mno katika kalenda ya mbinguni. Mojawapo ya hayo maandiko ya kibiblia yanajitokeza kuahidi kwamba siku ya *unyakuzi* itakuwa siku ya *kisiri* ya hali ya juu sana na *fiche,* ambayo kisawe chake hakiwezi kusawazishwa na kikingine chochote ila na mwizi anayekuja kuiba katikati mwa usiku (Ufunuo 16:15). Vivyo hivyo , baadhi ya yale maandiko mengine yanayo nakili matukio wakati wa unyakuzi, yameendelea kuelezea ile kasi kushinda kifani ambayo unyakuzi unatendeka kama inayotoshana na ghafla,kufumba na kufumbua jicho (1 Kor 15:50-56).Hata hivyo, Andiko la kipekee zaidi ambalo kwa wazi linadhihirisha utaratibu na itifaki ya jinsi unyakuzi utakavyotendeka ni kitabu cha Wathesalonike wa Kwanza Mlango wa 4 Mstari wa 16 hadi 17.

> 16 Kwa maana Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni, akitoa amri kwa sauti kuu pamoja na sauti ya malaika mkuu na sauti ya tarumbeta ya Mungu, nao wale waliolala mauti wakiwa wanamwamini Kristo watafufuka kwanza.
> 17 Baada ya hilo sisi tulio hai bado, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili kumlaki Bwana hewani, hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.
> (1 Wathesalonike 4:16-17).

## SAUTI KUBWA YA MUNGU

Hili andiko la muhimu linatoa taswira bayana ya matukio wakati wa *unyakuzi* kama vile ilivyodhihirishwa katika hayo maono ya hapo juu, ya Mei 17 2004. Tunaweza kuona ya kwamba baada ya matukio tangulizi, BWANA Yesu MWENYEWE Atashuka chini kihalisia kutoka mbinguni kulichukua kanisa lake takatifu. Lakini kabla ya BWANA MWENYEWE kushuka chini kuwachukua wateule WAKE watakatifu, ni lazima mbingu kwanza zimweka hadi urejesho wa vitu vyote. Baada ya *urejesho* wa vitu vyote, uliotangazwa katika biblia, ndipo BWANA Yesu Atakapotokea katika utukufu WAKE, ingawaje mara hii ,sio jinsi Alivyofanya katika Kujiwasilisha KWAKE kwa kwanza. Ijapokuwa Alijiwasilisha mara ya kwanza katika njia ya *upole* na *unyenyekevu* katika hori ya ng'ombe ya Bethlehemu, lakini kuja KWAKE kwa *unyakuzi* si kwa unyenyekevu kwa vyovyote vile. Huku kujiwasilisha kwa BWANA badala yake kutakuwa kwa *ufahari* mkuu na *nguvu* kiasi chake hakijawai kuonekana tangu kuumbwa kwa dunia. Tunaweza kuona kwa wazi ya kwamba katika haya maono ya *unyakuzi* ya Mei tarehe 17 mwaka wa 2004, kabla ya BWANA kujitokeza angani, kulikuwa na sauti kubwa ya MUNGU MKUU MWENYEZI, ikifuatwa na sauti ya Malaika Mkuu na kisha mwito wa MUNGU wa Tarumbeta. Kwa biblia kusisitiza kwamba BWANA MWENYEWE Atakuja na hayo matukio ya matangazo tangulizi, kimsingi Anamaanisha kwamba hayo matukio tangulizi yatakuwa matukio ambatani yakishughulikia kujiwasilisha kwake. Na kwa kusisistiza kupazwa kwa Sauti ya MUNGU kutoka mbinguni kabla ya Masihi kutokea, tunaweza kuona kwa wazi kwamba BWANA Anaashiria swala kwamba ile sauti kuu iliyopazwa inapaswa kuwa ishara kwamba Mfalme Anakuja na *nguvu* na *mamlaka*. Sauti kuu ya MUNGU imekusudiwa kudhihirisha mamlaka ya MSHINDAJI anayekuja. Ni muhimu kuzingatia kwamba katika maono haya, wakati BWANA Anapojiwasilisha, jambo la kwanza Analotenda ni kutengeneza TAJI YAKE YA UTUKUFU ILIYOPAMBWA KWA UZURI, ambayo inapeana ujumbe wazi kwa mataifa juu ya swala kwamba mara hii Anakuja kama MFALME MSHINDI NA MSHINDAJI. Basi amri ya MUNGU inapaswa kutoa agizo kwa majeshi wa mbinguni wanaomwandama ya kwamba na wakajiandae kwa ajili Anatoka nje. Pia ni amri ambayo kimsingi inapeana maagizo kwa majeshi wa mbinguni wanaomhudumia kujua kwamba hatua ya mwisho ya *mashambulizi* YAKE *ya mwisho* na *ushindi* dhidi ya dhambi, iko njiani.

## SAUTI YA MALAIKA MKUU

Katika maono haya ya Mei tarehe 17 mwaka wa 2004, wakati sauti ya Malaika Mkuu ilijitokeza, Alipaaza sauti kuu katika upande wa mkono wa kulia huku akisema,

> "TAZAMA! BWANA YU KARIBU KUJIWASILISHA ANGANI."

Tunaweza kuona kwamba sauti ya Malaika Mkuu iliyokuja kabla ya Masihi kujiwasilisha angani, kimsingi ilikusudiwa kuwaita malaika wa mbinguni wasiohesabika ambao watamshughulikia katika siku hiyo Anapowarudia *wateule takatifu*. Katika njia hii, Malaika Mkuu atapeana ilani ya kukaribia na *kujitokeza* kwa utukufu kwa *Mkombozi Mkuu* na *Hakimu.*

## TARUMBETA YA MUNGU

Baada ya tangazo la Malaika Mkuu ya kwamba BWANA yu karibu kujiwasilisha angani, tunaweza kuona kwa wazi kwamba, ni tangazo ambalo zaidi ya hapo linatangazwa na mwito wa TARUMBETA ya MUNGU.

Kwa maana wakati TARUMBETA itapigwa, jukumu lake ni kuwaaamsha wafu katika Kristo Yesu . Hawa ni Wakristo walio katika mavumbi ya dunia na hivyo basi wanaitwa na milio ya TARUMBETA ya MUNGU. Huu mwito wa TARUMBETA ndio ule ule mlipuko wa TARUMBETA ambao huwa unaandamana na ufunuo wa MUNGU wakati yeye MWENYEWE Anashuka chini katika utukufu wa Uwezo WAKE. Pia tunaweza kuona kwamba hapo mwanzoni, huu mlio wa TARUMBETA ulitumika kuwakusanya watu wa MUNGU Israel, katika kusanyiko takatifu wakati ambao YEHOVA MWENYEWE Aliamua kushuka kutoka mbinguni na kuwatembelea juu ya Mlima Sinai.

> 16 Asubuhi ya siku ya tatu kulikuwa na ngurumo na radi pamoja na wingu nene juu ya mlima na mlio mkubwa sana wa tarumbeta. Kila mmoja aliyekuwa kambini akatetemeka. (Kutoka19:16).
> 5 Mungu amepaa katikati ya kelele za shangwe. BWANA katikati ya sauti za tarumbeta. (Zaburi 47:5).
> 2 "Tengeneza tarumbeta mbili za fedha ya kufua, uzitumie kwa kuita jumuiya pamoja na wakati wa kuvunja makambi ili kuondoka. Hesabu 10:2).

Tangu jadi imekuwa desturi ya MUNGU kutumia mlio wa TARUMBETA kuwaita jamii ya Israel Pamoja ili wawe na *kusanyiko takatifu*. Hapa pia katika haya maono, tunaweza kuona kwamba BWANA Anatumia mlio wa TARUMBETA YAKE ili kuwakusanya wateule wa MUNGU katika hatua kuu ya maandalizi kwa ajili ya *kutukuzwa* kwao *unyakuzi* unapoanza.

> 8 Tena kama tarumbeta haitoi sauti inayoeleweka, ni nani atakayejiandaa kwa ajili ya vita? (1 Kor 14:8).

## BWANA MWENYEWE

Kwa kutangaza kwamba BWANA MWENYEWE katika siku hiyo Atashuka chini, maandiko kimsingi yanaashiria kwamba katika siku ya *unyakuzi*, BWANA Atashuka chini katika *ukuu* na *Uwepo* binafsi kama ilivyoonekana katika maono haya, na hatayakabidhi kwa mjumbe yeyote wa mbinguni. Kwa maneno mengine katika hafla hii BWANA hatakabidhi chochote kwa malaika, au kwa Roho wa BWANA, lakini Anakusudia kushika hatamu MWENYEWE kibinafsi inapofikia huko *kuteka nyara* kwa saa sita za usiku, kwa bi harusi wa kifalme. Atashuka kutoka mbinguni na kuja hewani na angaa juu ya ardhi, ili kutimiza hilo jukumu la kibinguni linalo dhaminiwa. Inashangaza kwamba BWANA Yesu Alipanda juu mbinguni baada ya kufufuka KWAKE na akapitia takita zile zile mbingu hadi katika mbingu za juu zaidi ya juu. Katika njia iyo hiyo wakati wa unyakuzi, YEYE MWENYEWE Atapita katika hizi mbingu ili kuja chini angani kukutana na kanisa la utukufu. Hata hivyo hili halitakuwa tukio nyamavu la kirahisi, ila litakuwa tukio kuu la kifahari na nguvu kuu kutoka mbingu za juu zaidi. Atashuka angani juu ya dunia sawa na Alivyopaa wakati wa kufufuka.

> 11 wakasema, "Enyi watu wa Galilaya, mbona mnasimama mkitazama juu mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda Mbinguni, atarudi tena jinsi iyo hiyo mliyomwona akienda Zake Mbinguni." (Matendo 1:11).

Na basi, wakati siku hiyo ya *unyakuzi* itakapotimia, BWANA Yesu Masihi, Atashuka chini kutoka mbinguni katika njia ili ile Aliyopaa. Haya maono yanafanyika mazungumzo ya muhimu sana ya *kiashiria,* yanayodhibitisha imara kwamba biblia ni ya kweli na sasa inatimizwa.

## WAFU KATIKA KRISTO WANAFUFUKA

Wafu katika Kristo ni wale waliolala katika Kristo Yesu. Na katika kesi hii,bila shaka tunaweza kuona kwamba mauti haiwaangamizi kwa sababu *wamelala* tu na wamejipata katika pumziko lisilo na mikosi. Kimsingi hawa Wakristo wamejiuzulu kutoka katika ulimwengu huu wa *matatizo* ili kupumzika kutoka kwa *masumbuko* na *mateso yao* wanapopumzika katika Kristo Yesu. Kwa hiyo,wakiwa bado katika ushirika na Kristo, na muungano NAYE wanalala chini ya ulinzi na utunzaji WAKE maalum na katika kufanya hivyo, nafsi zao ziko katika Uwepo WAKE na chini ya nguvu zake kiasi ya kwamba hawapotei wala si wapotezaji. Badala yake, wao ni *wafaidikaji* wakuu katika mauti, na kuondolewa kwao kutoka duniani ni kwa faida yao. Basi ni wao watakaoinuliwa kutoka kwa wafu na kuamushwa kutoka kwa usingizi wao. Hii injili ya kufufuka kwa wafu wakati wa kuja kwake Kristo, ndio inayofanyika pingamizi kuu dhidi ya hofu ya kifo ambayo mara nyingi huwakumba wanaume na wanawake , na pia watoto. Kwa maana Kristo MWENYEWE Akiwa Amefufuka kutoka kwa wafu Amefanyika malimbuko kati ya wale waliolala.

> 20 Lakini kweli Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, tunda la kwanza la wale wote waliolala (1Kor 15:20).

Kwa hiyo,maono haya yanasisitiza kwamba wale walio wafu katika YEYE ama kweli hawajapotea wala kuangamia. Kufufuka kwa Kristo kumefanyika dhibitisho na kipimio dhabiti cha yote Alioyasema katika injili. Na basi neno la MUNGU limeleta *nuru* na *kutokufa* maishani kama Alivyoahidi. Hiyo yaweza tu kumaanisha kwamba hali ya kuwa wamelala katika Kristo, yaweza tu kuboreka kwa sababu katika siku hiyo ya *unyakuzi* watakuwa wa *utukufu* na wenye *furaha zaidi* wakipokea miili yao ya milele isiyoharibika. Kwa hiyo, kutoka kwa maono haya tunaona kwamba wafu katika Kristo ni wale Wakristo ambao wakati wao wa kufa walikuwa wakiiishi maisha ya *kutubu* ya *utakatifu* na *uhaki*. Haiashirii kwa vyovyote vile wakristo wote waliokufa, lakini inaelekeza moja kwa moja kwa wale tu ambao katika mtembeo wao wa ukristo , walikuwa wakifuatilia sana *uhaki*, *utakatifu* na *utauwa* unaohitajika.

## WALE WALIO HAI

Kama vile maandiko yanavyoelezea, wateule wafu katika Kristo basi *watafufuliwa*, *watainuliwa* na kupewa miili ya milele, ya utukufu kwanza, kabla ya hao Wakristo watakatifu walio hai kugeuzwa. Lakini,wale Wakristo watakatifu watakao kuwa hai wakati huo wa unyakuzi itawapasa kutekeleza tunuku na heshima ya kugeuzwa kabisa kabisa ambayo kwa kweli inasawazishwa na kufa na kufufuka.






Hii ni kwa sababu itawapasa wabadilishwe kutoka katika nyanja hii ya kufa hadi ile nyanja ya BWANA ya *kutokufa*, na kutoharibika. Katika njia hiyo,itawapasa wageuzwe kutoka kwa miili yao ya kufa kuwa miili ya mbinguni isiyokufa. Ni lazima hapa kutaja swala kwamba haya mabadiliko ni ya kisiri ajaabu sana kiasi kwamba hakuna mwanadamu awezaye kuelewa katika nyakati hizi. Mwili huu wa kufa itabidi ukapitie kubadilishwa kuu sana kuwa wa kutokufa, ambao hii mwili na damu ya sasa haiwezi kufikia.

51 Sikilizeni, nawaambia siri: Sote hatutalala, lakini sote tutabadilishwa (1 kor 15:51).

Hivyo, wale wote watakaochukuliwa kwa *unyakuzi* kimsingi watakutana na BWANA angani mawinguni ili Awape hongera kwa kazi njema waliotenda. Sana sana, hapa ndipo karamu ya kudhawabiwa sawa sawa na yale walioyatenda, itatendeka. Kisha wafu watakatifu watapokea taji zao za utukufu katika karamu itakayokuwa furaha kubwa ya wale wote watakaonyakuliwa watakapokutana na BWANA ana kwa ana. Na biblia inaposema kwamba tutakuwa pamoja nao, kimsingi BWANA Anazungumzia kuungana kwa wafu wafufuliwa na Wakristo hai wafufuliwa ili kutengeneza mwili mmoja wa wateule wa MUNGU wa unyakuzi.

## MAWINGUNI

Katika siku ya *Unyakuzi,* MUNGU wa mbinguni Atawakabidhi wateule watakatifu heshima ile ile Aliyokabidhiwa BWANA wetu Yesu. Sawa na Alivyochukuliwa juu mawinguni wakati wa kupaa kwake, ndivyo watakatifu walionyakuliwa watakavyochukuliwa juu katika wingu la kupaa kwao.

9 Baada ya kusema mambo haya, walipokuwa wanatazama, akachukuliwa juu mbinguni mbele ya macho yao na wingu likampokea wasimwone tena. (Matendo1:9).

Kwa hakika ni ya ajaabu na ya kushangaza kabisa kwamba hili ndilo lile lile wingu ambalo BWANA Atarudi nalo Yerusalemu baada ya unyakuzi, tunapokaribia zaidi mwisho wa dahari.

7Tazama! Anakuja na mawingu
na kila jicho litamwona,
hata wale waliomchoma mkuki,
na mataifa yote ulimwenguni
yataomboleza kwa sababu yake.
Naam ndivyo itakavyokuwa!
Amen. (Ufunuo 1:7).

Haya mawingu kwa kweli ni milki ya BWANA pamoja na magari ya ushindi yatakayo kuwako wakati wa kurudi KWAKE.

3 na kuziweka nguzo za orofa yake juu ya maji. Huyafanya mawingu kuwa gari lake kubwa zuri, na hupanda kwenye mbawa za upepo. (Zaburi 104:3).

## KUKUTANA NA BWANA HEWANI

Wakati maandiko yanasema kwamba *tutakutana* na BWANA hewani, kimsingi inamaanisha kwamba wateule wote *watakaonyakuliwa* watakusanywa katika maeneo yaliyo juu tu ya ardhi na hapo ndipo mahali pale ambapo *mkutano* kati ya BWANA na wateule utatendeka. Katika Mathayo 25:1, bila shaka tunaona kwamba wateule watakatifu ambao wanasimamiwa na wanawali wenye busara wanatoka nje kwenda *kumlaki* bwana harusi. Hili ni kanisa takatifu lililo na upako wa Roho Mtakatifu anayesimamiwa na kile *chombo cha mafuta* ili wakaweze kutembea. Lakini la muhimu sana katika mtembeo wao ni kwamba wanatoka nje kwenda *kumlaki* bwana harusi.

25 "Wakati huo, Ufalme wa Wakati huo, Ufalme wa Mbinguni utakuwa kama wanawali kumi waliochukua taa zao na kwenda kumlaki bwana arusi. (Mathayo 25:1).

Katika njia hii, BWANA Anasema kwamba wateule watakuwa *wakipanda* huku naye BWANA *Akishuka,* ili wakutane hewani juu ya ardhi.Kimsingi wateule watakuwa wakipanda kwenda mbinguni naye BWANA Akishuka kuelekea duniani hadi wakutane hewani hapa juu.

6 "Usiku wa manane pakawa na kelele: 'Tazameni, huyu hapa bwana arusi! Tokeni nje mkamlaki!' (Mathayo 25:6).

Aidha, BWANA Aliposema, 'Na basi tutakuwa na BWANA siku zote.' Ilifanyika ishara nyingine ya kwamba baada ya unyakuzi, hapatakuwepo tena na kutengana kati ya wateule na BWANA. Ukizingatia kwamba wanawali wenye hekima walitoka nje kukutana na BWANA,basi hii kimsingi inamaanisha kwamba hakutakuweko na kutoka nje tena.

12 Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo kamwe. Nitaandika juu yake Jina la Mungu wangu na jina la mji wa Mungu wangu, yaani, Yerusalemu mpya, ambao unashuka kutoka mbinguni kwa Mungu wangu. Nami pia nitaandika juu yake Jina langu jipya. (Ufunuo 3:12).

Jambo la muhimu zaidi likiwa kwamba mahali hapa, wafu katika Kristo watakuwa na fursa ya manufaa sawa na wale ambao Masihi Atawapata wakiwa hai na watakatifu. Na basi, kulingana na maono haya ya unyakuzi wa watakatifu ya Mei tarehe 17 mwaka wa 2004, tunaweza kuona ya kwamba kwa kweli yalikuwa mazungumzo ya kina sana na bibi harusi wa Kristo. Na kutakuwepo na *amri kuu* ya MUNGU, ikifuatwa na *sauti ya Malaika Mkuu*, na kisha *mlio* mkuu wa *TARUMBETA* ya MUNGU. Baada ya hapo BWANA MWENYEWE Atashuka chini kutoka mbinguni huku wateule watakatifu na wenye haki wakipanda kuelekea mbinguni, na watakutana mawinguni hewani juu ya ardhi, na BWANA na wateule *walionyakuliwa* watakuwa pamoja milele katika ufalme wa MUNGU wa utukufu. AMINA. ▪